

1. **Teknolojia asilia ya Wasukuma ya kuhifadhi uoto wa asili na malisho ya *Ngitili*: Uzoefu wa Mkoa wa Shinyanga.** Rubanza, C.D.K., Bakengesa, S.S., Minja, E., Machanya J., Mlenge, W. 2008.

#### **Muhtasari**

Kutenga maeneo ya malisho ya kiasili kama *Ngitili* ni mojawapo ya mkakati wa kuzuia ufugaji wa kuhama hama kwa kuwa *Ngitili* huweza kutoa malisho bora kwa misimu yote ya mwaka iwapo matumizi endelevu yata zingatiwa. Makala haya yanabainisha teknolojia ya asili ya kutenga malisho ya asili ya '*Ngitili*' ifanywavyo na Wasukuma, au kama inavyo julikana miongoni mwa jamii nyingine za wafugaji, mfano, 'Ekiriro' (Wakurya), 'Obulisizo' (Wahaya), 'Oliriri' (Wamasai), 'Kibawo' (Warangi), 'Ndobido' (Wanyaturu), n.k. Dhana ya hifadhi ya uoto wa asili iliyo boreshwa kwa kutumia teknolojia mbali mbali za kilimo mseto/misitu, kwa mfano, urutubishaji wa malisho ya *Ngitili* kwa kupanda miti ya kuongeza rutuba hii ikiwa ni pamoja na miti malisho ya asili: Mi-akasia (Mihale, Migu na Migunga), Miti malisho ya kigeni (Lusina, Gliricidia, Calliandra, Sesbania, nk), na kayamba (*Desmodium lablab*) inastahili kuigwa kitaifa. Kuna nafasi pia ya kuboresha malisho ya asili kwa kupanda aina za nyasi bora zenye tija mkubwa. Hata hivyo uzalishaji wa malisho ya *Ngitili* unaweza kuboreshwa zaidi iwapo mipaka ya mashamba ya wakulima itaimarishwa kwa kutumia teknolojia husika za kilimo misitu ikiwa ni pamoja na miti ya mipaka yenye manufaa mbali mbali, mfano kurutubisha udongo, kivuli, kuzuia upepo, kutoa mbao, n.k. Matumizi endelevu ya *Ngitili* yatafikiwa kutegemeana na sheria ndogo ndogo zilizowekwa/zitakazo wekwa kusimamia kutunza na ulishaji/ kuchunga kwenye maeneo ya malisho ya asili ya *Ngitili*. Makala haya yanabainisha sheria za kutenga maeneo ya hifadhi ya uoto wa asili wa *Ngitili* kwa ujumla, sheria zinazo simamia ulishaji wakati wa kiangazi kwa kutumia dhana shirikishi baina ya wadau husika kwa kutumia uzoefu wa Mkoa wa Shinyanga. Hata hivyo changamoto zinazo ikabili sekta hii ya hifadhi ya maliasili kupitia uoto wa asili na malisho ya asili ni pamoja na ukosefu wa hati miliki, uelewa mdogo miongoni mwa wadau juu ya umuhimu wa hati miliki ya uoto wa *Ngitili*, na mlolongo mrefu wa kupata hati miliki. Changamoto zingine ni pamoja na ukosefu wa kipimo sahihi cha thamani ya maliasili ikiwa ni pamoja na malisho ili kutumika kama amana inayoweza kukubalika na taasisi za kifedha (benki) za kuweka na kukopa ili kuwainua wakulima/ wafugaji.

2. **Mchango wa *Ngitili* katika kupunguza umasikini wa kipato Busongo Shinyanga, Tanzania.** Nkwilima, E.M. and Rubanza, C.D.K. 2008.

#### **Muhtasari**

Utafiti uliofanyika hapa Shinyanga unaonyesha kuwa pamoja na misitu ya asili kuendelea kupungua kadri muda unavyopita, mazao ya misitu na miti kutoka katika misitu ya jamii iliyohifadhiwa inaendelea kuwa ni chanzo kikubwa cha mahitaji ya lazima ya watu ikiwa ni pamoja na mazao ya kilimo na vyanzo vingine. Misitu hiyo inayohifadhiwa kwa njia ya asili ya Wasukuma ijulikanayo kwa jina la **“Ngitili”** imekuwa ni ya msaada mkubwa sana kwa jamii ya watu waishio vijijini katika Mkoa wa Shinyanga. Umuhimu wa misitu hiyo huwa bayana wakati wa kipindi cha upungufu wa chakula, na kiangazi kwa ajili ya malisho. Katika utafiti imedhihirika kuwa asilimia 14 ya mapato ya fedha taslimu katika ngazi ya kaya inatokana na mazao ya misitu wakati asilimia 44 ya matumizi yote ya nyumbani yanatokana na mazao ya misitu. Hata hivyo mazao ya misitu kwa ujumla katika jamii ya Kijiji cha Busongo yanachangia kiwango cha asilimia 29.

### **3. Usimamizi shirikishi wa misitu ya jamii na changamaoto zake. Machanya, J . 2008.**

#### **Muhtasari**

Usimamizi wa rasilimali za Misitu na Maliasili kwa ujumla hapo nyuma ulikuwa chini ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa au Taasisi ambazo nyingi zilikuwa chini ya serikali. Utaratibu huu ulitokana na mambo mengi ikiwemo fikra za wakati huo zilizokuwa hazithamini sana mchango wa wananchi. Hali hii haikuwa kwenye sekta ya maliasili tu, bali karibu sekta zote ambapo shughuli za uzalishaji na huduma zilionekana kwa jamii kwamba ni za serikali. Mipango ya maendeleo ya jamii ilipangwa na makao Makuu ya Wizara kwa upande wa Serikali Kuu au na Wilaya kwa upande wa Serikali za Mitaa. Umma/jamii iliyopangiwa mipango hiyo ya maendeleo haikushirikishwa ipasavyo, hivyo iliiona mipango, na maendeleo yaliyotarajiwa kupatikana kuwa ni ya serikali. Hali hii ilidumaza maendeleo na pale mafanikio yalipopatikana jamii haikujivunia kwani haikuwa na mamlaka na kile kilichopatikana. Mabadiliko ya kisiasa, kijamii na kiuchumi yaliyotokea katika miaka ya 1980/1990 yalizifanya nchi nyingi duniani zibadili mwelekeo wao wa kisiasa na kiuchumi. Tanzania kwa upande wake ilifanya marekebisho ya sera kuu ya uchumi wa taifa ilibainika kuwa ipo haja ya kushirikisha wadau wote katika kufanya maamuzi ya kupanga mipango, na katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ya sekta ya maliasili na sekta ndogo ya Misitu na Ufugaji wa Nyuki. Marekebisho ya sera kuu ya uchumi wa taifa na ushirikishwaji wa wadau, yamepelekea kufanyiwa mapitio kwa Sera ya Misitu na kuundwa upya kwa Sera ya Ufugaji Nyuki. Mapitio haya yamezingatia ushirikishwaji wa wadau katika ulinzi, uendelezaji na utumiaji wa rasilimali zitokanazo na misitu. Hivi sasa programu nyingi za misitu ya jamii zimeanza kuchukua sura mpya ya kushirikiana na wadau wote katika utunzaji, ulinzi na matumizi ya rasilimali ya mazao na huduma za misitu ili ziwe endelevu. Ushirikiano wa wadau katika kusimamia Misitu na Ufugaji wa Nyuki umeonyesha mafanikio makubwa katika matumizi endelevu ya mazao na huduma pamoja na kuongeza kipato cha jamii ili kuendana na marekebisho ya sera kuu ya uchumi wa taifa, kuingiza dhana ya ushirikishwaji wa wadau, kufanya matumizi endelevu na kuimarisha mchango wa

sekta ndogo ya Misitu na Nyuki katika kuleta maendeleo endelevu kwa Taifa, Idara ya Misitu na Nyuki ilitoa mwongozo wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu (USM).

4. **Kilimo misitu na uhifadhi wa mazingira. Bakengesa, S.S., Rubanza, C.D.K. and Iddy, O.D. 2008.**

#### **Muhtasari**

Kilimo mseto/ kilimo misitu ni utalaamu ambao uoteshwaji mazao ya chakula na misitu au miti hupishana au unakuwa sambamba; kama ilivyo kwa mazao ambayo ni malisho ya wanyama, na miti; miti ya kurutubishayo ardhi na hifadhi ya mazingira. Teknolojia zote hizi huweza kutumika kwa pamoja katika sehemu moja ya ardhi au eneo la ardhi lililo karibu lillitengwa kwa ajili ya mifumo mbali mbali ya kilimo mseto. Teknolojia hii huongeza uzalishaji/ tija kutokana na uwezo wa mchanganyiko huu wa mimea kurutubisha ardhi. Rutuba ya ardhi huboreshwa zaidi pale ambapo samadi inatawanywa mashambani. Utaalamu wa Kilimo Mseto unatoa fursa ya kueneza na kudumisha teknolojia mbali mbali ambazo zinachangia katika uboreshaji uhakika wa chakula, kuondoa umasikini na kufanya mazingira yatumike kwa uendelevu. Kilimo mseto ni mbinu rahisi ya kukoresha uharibifu wa mazingira unaotishia karibu maeneo mengi ya nchi (NASCO, 2006). Mtazamo wa uzalishaji wa sasa umelenga na kujikita kwenye teknolojia za Kilimo Mseto kutokana na mbolea za viwandani kuuzwa kwa bei kubwa kiasi cha wakulima walio wengi kushindwa kuzinunua. Upatikanaji wa mbolea za viwandani ni mgumu sehemu za vijijini kutokana na kuwa na mapungufu ya miundombinu.

5. **Agroforestry tree products for household income and poverty reduction in semi-arid areas of Misungwi District, Mwanza Tanzania. Maduka S. M. and Kessy J. F. 2008.**

#### **Abstract**

Agroforestry products like any other; have been reported to play a role in contributing to household incomes and reducing poverty. This study was conducted in order to examine how agroforestry products contribute to total annual household incomes and poverty reduction in semi-arid areas of Misungwi District, Mwanza Tanzania. Research methodologies used included literature review, questionnaire administration, discussion with key informants and personal observations. For questionnaire surveys, a sample of 127 households engaged in agroforestry and non-agroforestry practices was randomly selected from six villages. Data analysis involved content analysis and use of SPSS computer program. The agroforestry technologies practiced in the area included woodlots (38%), boundary planting (4%), *Ngitili* (15%) and indigenous live fence (21%). Agroforestry products and benefits that mainly generated from woodlots were poles (80%), fuelwood (86%), timber (92%) and thatch grasses (33%). There is a potential market for agroforestry products, particularly for poles which contributed about TShs 159,000.00 (127 US\$) equivalent to 6% of the annual total

household income. However, this contribution is lower than contributions from agriculture and livestock keeping. Through regression analysis, tree products to total households income was not statistically significant at  $p < 0.05$  but positively correlated to total annual household incomes while agriculture and livestock keeping were statistically significant at  $p < 0.01$ . In comparison, agroforestry practitioners were richer than non-participants with extra income of TShs 954,611.00 (760 US\$) per year. This study concludes that agroforestry practice in the District provide minimal contribution to the total annual household income because it is constrained by modest amount of trees planted, lack of education and perverted selling prices. The study recommends agroforestry practice to be enhanced as alternative sources of income generating activity in the District as a contribution to National Strategy for Growth and Poverty Reduction, and Millenium Development Goals

